CHUO KIKUU CHA SOKOINE
CHA KILIMO

# MATUKIO YA SUA

*Aprili - Juni, 2026*



*Toleo la 22*

**Ardhi ni Hazina**

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| 1 | Bodi ya Uhariri |
| 2 | SUA yaandika rekodi ya kipekee kwa CAG kwa miaka 20 mfululizo. |
| 4 | Mapinduzi ya kilimo: SUA na AgriMazao wapiga msasa wanafunzi matumizi ya droni Morogoro |
| 5 | SUA yahamasisha ubunifu na tafiti za kilimo |
| 6 | Teknolojia za GIS na picha za satelaiti zasaidia upangaji endelevu wa miji: SUA na Westminster zaimarisha ushirikiano |
| 7 | • Wanafunzi SUA watakiwa kutumia elimu waipatayo ili kujiajiri<br>• Vyuo vya elimu ya juu kuwawezesha vijana kupata maarifa, ujuzi na fursa za kiuchumi kupitia ubunifu na ujasiriamali |
| 8 | DC Mongera apongeza ubunifu wa SUA Kampasi ya Mizengo Pinda wiki ya nyuki Tabora |
| 9 | SUA yazindua kitabu |
| 10 | Serikali yaipongeza SUA kwa mchango wake katika kuendeleza kilimo Ikolojia nchini |
| 11 | Watafiti wa mradi wa NANOCOM watembelea wafugaji wa maziwa tanga kuimarisha sekta ya mifugo |
| 12 | Wataalamu wahimizwa matumizi ya kilimo ikolojia waonya athari za kemikali za kilimo |
| 13 | • SUA Yaimarisha Mafunzo kwa Vitendo kwa Wanafunzi wa Teknolojia ya Mbao<br>• Mafunzo kwa vitendo katika sekta ya uvuvi yaimarisha ujuzi kwa wanafunzi wa SUA |
| 14 | SUA yaimarisha ujuzi wa kidijitali kwa wanafunzi na watumishi wa kilimo biashara |
| 15 | • Ndege nyuki kuwasaidia wanafunzi SUA kujifunza katika mazingira halisi ya kiteknolojia<br>• Wanafunzi Mafiga Sekondari wapongeza SUA kwa kuimarisha mafunzo ya amali |
| 16 | Serikali inaendelea kuweka mazingira rafiki ya kuwawezesha vijana kiuchumi, Waziri Nanauka |
| 17 | SUA, AFIDA na IFA watoa mafunzo ya mbolea endelevu kuimarisha kilimo Afrika |
| 18 | Wanafunzi wa udaktari wa mifugo SUA wapata mafunzo kwa vitendo katika uhifadhi wa wanyamapori |
| 19 | Tathmini mapato ya kaboni yaangaliwa kama njia endelevu ya kufadhili uhifadhi wa misitu ya jamii Tanzania |
| 20 | SUA na Messina wapo hatua ya mwisho kuanzisha Programu pacha |
| 21 | Waziri Kabudi asisitiza umuhimu wa kuimarisha huduma za afya ya uzazi, elimu na utafiti katika taasisi za elimu ya juu |
| 22 | Wajumbe wa Baraza SUA wajengewa uwezo kuimarisha uongozi na uatawa bora |
| 23 | Watumishi wa SUA wakumbushwa kuweka akiba na kuwekeza kwa ajili ya maisha ya baadaye |
| 24 | Ushirikiano wa SUA na APOPO waendelea kukua, maabara ya muda ya uchunguzi wa kifua Kikuu yapendekezwa kujengwa Olmontonyi |
| 25 | Wanafunzi SUA wahimizwa kupima afya mara kwa mara kujua hali zao |




## WATAALAMU WA MAWASILIANO NA MASOKO

**Bi. Suzana Magobeko**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko

**Bw. Asifiwe Mbembela**
Afisa Mawasiliano na Masoko


## MHARIRI

**Prof. James Nyangas**
Mkuu wa Idara ya Elimu ya Saikolojia na Unasihi

## WASANIFU

**Bw. Rajab Kimaro**
**Bi. Jackline Japhet**





*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda akiongea wakati wa Mahafali ya 47.*

# SUA yaandika rekodi ya kipekee kwa CAG kwa miaka 20 mfululizo

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimeandika historia kwa kupata Hati Safi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka 20 mfululizo, mafanikio yanayoakisi uwajibikaji, uwazi na usimamizi madhubuti wa rasilimali za umma.

Mafanikio hayo yalitangazwa wakati wa Mahafali ya 47 ya Chuo hicho yaliyofanyika katika Kampasi ya Edward Moringe, Morogoro ambapo SUA iliendelea kuadhimisha uwezo wake katika usimamizi wa fedha

Mbali na kupata Hati Safi kwa miaka 20 mfululizo, Chuo pia kimeendelea kufanya vizuri katika uaandaaji wa taarifa za fedha baada ya kutunukiwa tuzo ya Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) kama taasisi bora ya elimu ya juu nchini katika uandaaji wa hesabu za fedha kwa miaka mitatu mfululizo.

Mahafali hayo yalipambwa na kuhitimu kwa jumla ya wahitimu 877 waliotunukiwa Shahada za Uzamivu, Uzamili, Shahada za Awali, Stashahada na Astashahada chini ya uongozi wa Mkuu wa Chuo, Jaji Joseph Sinde Warioba.

Akiwasilisha taarifa ya mafanikio ya Chuo katika eneo la fedha na utawala bora, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda, alisema mafanikio hayo yametokana na kuimarika kwa mifumo ya usimamizi na uwajibikaji ndani ya Chuo.

"Tumeimarisha nidhamu katika utekelezaji wa majukumu ya Chuo, na hatua hiyo imetuwezesha kuendelea kupata hati safi kutoka kwa CAG," alisema Prof. Chibunda.

Prof. Chibunda alibainisha kuwa wahitimu 877 walitoka katika programu 83 za masomo, ambapo wanaume walikuwa 517 na wanawake 360.



***Mhe. Andrew Massawe***
***Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.***

## *Picha za matukio mbalimbali wakati wa Mahafali ya 47 ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo 21 Mei, 2026.*


















# Mapinduzi ya kilimo: SUA na AgriMazao wapiga msasa wanafunzi matumizi ya droni Morogoro

Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kimepiga hatua nyingine kubwa katika kuandaa wataalamu wa kilimo cha kisasa baada ya kuendesha mafunzo ya vitendo ya teknolojia ya ndege nyuki (droni) kwa wanafunzi wote wanaosomea fani mbalimbali za kilimo na ufugaji.

Mafunzo hayo yalifanyika kwa lengo la kuwapa vijana ujuzi wa jinsi ndege nyuki zinavyoweza kutumika kupulizia viuadudu, kufanya tathmini ya afya ya mazao, na ramani za kidijitali za mashamba.

Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda, akizungumzia uzito wa mafunzo hayo, alibainisha kuwa chuo kimefanya maamuzi ya makusudi kuwekeza kwenye teknolojia hiyo ili kuendana na dira ya Serikali ya Awamu ya Sita.

"Tumetenga bajeti kwa ajili ya kukuboresha jinsi tunavyofundisha wanafunzi wetu. Sisi kama wafundishaji hatuwezi kubaki nyuma, yaani tukaacha wahitimu wetu wakaenda kuona hivi vitu wanapokuwa wamemaliza chuo. Tumejipanga ili wawe waajiriwa bora, lakini sehemu kubwa wawe na ujuzi wa kwenda kujiajiri," alisema Profesa Chibunda.

Naye Rasi wa Ndaki ya Kilimo, Dkt. Nyambilila Amuri akifafanua kiufundi kuhusu umuhimu wa mafunzo hayo, alisema matumizi ya droni ni sehemu ya utekelezaji wa mitahala mipya inayolenga kilimo cha uhakika (Precision Agriculture).

"Matumizi ya droni yanaleta kilimo cha uhakika (precision agriculture). Tutaweza kutumia mbolea na viuatilifu kwa kiwango sahihi na kwa eneo sahihi, jambo linaloongeza tija na ufanisi wa pembejeo, huku tukikabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi kwa kufanya kilimo kiwe rafiki kwa mazingira."

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa kampuni ya Agri Mazao Mohamedi Salimu, alieleza kuwa ushirikiano wao na SUA unalenga kuwapa wanafunzi uzoefu wa vitendo kutoka sokoni.

Alibainisha kuwa droni zina uwezo wa kufanya kazi kubwa kwa muda mfupi, jambo ambalo ni mkombozi kwa mkulima katika kupunguza gharama za vibarua na dawa.



*Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda akizungumza na wanafunzi (hawako pichani) kushoto ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango, Fedha naUtawala Prof. Amandus Muhairwa.*







# SUA yahamasisha ubunifu na tafiti za kilimo

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma na Utafiti), Prof. Maulid Mwatawala, amesisitiza umuhimu wa kuwekeza katika tafiti na ubunifu wa kilimo ili kuongeza uzalishaji na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi.

Akizungumza katika kongamano la Ufadhili wa Miradi ya Maendeleo Nchini lililofanyika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), alisema tafiti za Chuo zinaendelea kutoa suluhisho kwa changamoto za wakulima, ikiwemo maendeleo ya mbegu bora za mpunga na maharage zinazohimili magonjwa na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Kongamano hilo liliwakutanisha wadau kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), wahadhiri na wanafunzi wa shahada ya umahiri.

Mkurugenzi wa TOSCI aliipongeza SUA kwa kuandaa kongamano hilo, akibainisha kuwa ushirikiano kati ya taasisi mbalimbali una mchango mkubwa katika kuimarisha tafiti zenye manufaa kwa wakulima na kuimarisha usalama wa chakula nchini.









# Teknolojia za GIS na picha za satelaiti zasaidia upangaji endelevu wa miji: SUA na Westminster zaimarisha ushirikiano

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimekaribisha ujumbe kutoka Chuo Kikuu cha Westminster cha Uingereza kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika tafiti, ubadilishanaji wa wataalamu na wanafunzi, pamoja na maendeleo ya teknolojia za upangaji miji.

Ujumbe huo uliongozwa na Mkurugenzi wa Programu ya Shahada za Uzamili ya Usanifu Miji (PG Urban Design), Dkt. David W. Mathewson, ukiwa na wanafunzi tisa wa shahada za uzamili pamoja na Profesa mwenzake, Dkt. Martin Mathews.

Akizungumza wakati wa mapokezi ya ujumbe huo, Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Shahada za Uzamili, Utafiti, Uhawilishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalam wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Japhet J. Kashaigili, alisema ushirikiano huo wa kimkakati utalenga kuendeleza tafiti za pamoja, usimamizi wa wanafunzi wa shahada za uzamili, uhawilishaji wa teknolojia, kubadilishana wataalamu na kuimarisha utoaji wa huduma za ushauri wa kitaalam kati ya taasisi hizo mbili.

Katika ziara hiyo, wajumbe walitembelea Ndaki ya Sayansi Asili na Tumizi (CoNAS), ambako walijionea shughuli mbalimbali za utafiti na matumizi ya teknolojia katika nyanja za mazingira, mipango miji na mifumo ya taarifa, kupitia maabara za kisasa zinazowezesha uchambuzi wa data kwa usahihi.

Mhadhiri kutoka Idara ya Infomatikia na Teknolojia ya Habari, Dkt. Theofrida J. Maginga, aliwaongoza wageni katika maabara mbalimbali na kuwaonesha jinsi wanafunzi wa SUA wanavyotumia teknolojia za GIS pamoja na picha za satelaiti kufuatilia mabadiliko ya matumizi ya ardhi na kusaidia maamuzi ya maendeleo endelevu.

Naye Dkt. Neema Sumari alisema tafiti alizozifanya katika miji ya Dodoma na Morogoro kwa kipindi cha zaidi ya miaka 20 zimeonesha kuwa matumizi ya teknolojia za GIS na picha za satelaiti yamechangia kwa kiwango kikubwa kuboresha upangaji wa ukuaji wa miji, usimamizi wa matumizi ya ardhi na kupunguza migogoro inayohusiana na ardhi.









# Wanafunzi SUA watakiwa kutumia elimu waipatayo ili kujiajiri




Wanachuo wa mwaka wa tatu wa Shahada ya Sayansi za Mazingira na Usimamizi katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo wametakiwa kutumia elimu na ujuzi wanaoupata chuoni kujiajiri na kuanzisha shughuli za kiuchumi zitakazonufaisha jamii kupitia teknolojia ya Juncao.

Akizungumza wakati wa mafunzo maalumu yaliyotolewa kupitia Mradi wa Teknolojia ya Juncao unaofadhiliwa na Serikali ya China nchini Tanzania, Rasi wa Ndaki ya Sayansi Asilia na Tumizi, Dkt. Geoffrey Karugila alisema teknolojia hiyo ni fursa muhimu kwa vijana kuanzisha miradi ya uzalishaji, biashara ndogo na za kati pamoja na kuibua ajira mpya.

Kwa upande wake, Kiongozi wa Timu ya Wataalamu wa Teknolojia ya Juncao, Bw. Wang Yunyong alisema ameridhishwa na namna wanachuo wanavyojituma katika kujifunza teknolojia hiyo inayohusisha kilimo cha uyoga, ufugaji, matumizi ya nyasi za Juncao kama chakula cha mifugo pamoja na urejeshaji wa ardhi iliyochoka. Aliahidi pia kutoa ajira za muda mfupi kwa baadhi ya wahitimu watakaojiunga na mradi huo wa miaka mitatu.

Dkt. Beda Mwangonde alisema zaidi ya vijana 80 wameshiriki mafunzo hayo yenye lengo la kuwawezesha kujiajiri baada ya kuhitimu masomo yao.

Mmoja wa wanachuo walioshiriki mafunzo hayo, Asifiwe Allen alisema mafunzo hayo yatawawezesha vijana kujitengenezea ajira kupitia uzalishaji wa uyoga na shughuli nyingine za kiuchumi.

Mradi wa Teknolojia ya Juncao wa miaka mitatu (2026–2029) unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

# Vyuo vya elimu ya juu kuwawezesha vijana kupata maarifa, ujuzi na fursa za kiuchumi



Naibu Makamu Mkuu wa Chuo cha Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) anayeshughulikia Mipango, Fedhan a Utawala Prof. Amandus Muhairwa amesema vyuo vya elimu ya juu nchini vipo tayari kushirikiana katika kuwawezesha vijana kupata maarifa, ujuzi na fursa za kiuchumi kupitia ubunifu na ujasiriamali.

Alisema hayo wakati wa uzinduzi wa Jukwaa la Vijana la Platform Campus Connect Mkoa wa Morogoro lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

“Vyuo vya elimu ya juu havipaswi kuwa maeneo ya kufundisha na kutoa vyeti pekee, bali ni vituo vya maarifa, ubunifu, utafiti na ujasiriamali unaowajenga vijana kuwa viongozi wa kesho", alisema.

Alisema jukwaa hilo limekuja wakati mwafaka, kwani vijana wa sasa wanazo fursa nyingi katika sekta za kilimo, teknolojia, masoko na uzalishaji, lakini wanahitaji taarifa sahihi, ujuzi wa kitaaluma, mitandao ya kibiashara na mazingira wezeshi ili kufanikiwa.





# DC Mongera apongeza ubunifu wa SUA Kampasi ya Mizengo Pinda wiki ya nyuki Tabora

Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Mhe. Gerald Mongera, amekipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Kampasi ya Mizengo Pinda kwa kuwa mstari wa mbele katika kuleta mapinduzi ya kiteknolojia kwenye sekta ya ufugaji nyuki nchini kupitia mafunzo ya vitendo na bidhaa bora.

Pongezi hizo alizitoa alipotembelea Banda la Kampasi hiyo katika Maadhimisho ya Wiki ya Nyuki Kitaifa yaliyofanyika mkoani Tabora kwenye Viwanja vya Kumbukumbu ya Vita.

Akiwa bandani hapo, Mhe. Mongera alielezwa mambo mbalimbali yanayooneshwa kwenye wiki hiyo na Bi. Carine Singu, mwanafunzi wa mwaka wa pili anayesoma Shahada ya Awali ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki (Bachelor of Science in Bee Resources Management).

Alisema kozi za kimkakati zinazotolewa chuoni hapo pamoja na kuonyesha vifaa vya kisasa vinavyotumika katika kujifunzia, uvunaji na uchakataji wa asali safi na mazao mengine ya nyuki.

Mhe. Mongera alivutiwa na namna Chuo kinavyochanganya nadharia na vitendo, hasa kwa kuona mizinga ya kisasa na vifaa vya uchakataji vinavyoandaliwa na wataalamu pamoja na wanafunzi wenyewe kupitia karakana na viwanda vya Chuo.

"Hivi ndivyo vyuo vyetu vinatakiwa kufanya. Siyo tu kutoa vyeti, bali kutoa wataalamu wenye ujuzi wa vitendo na uwezo wa kubuni vifaa vinavyoenda kutatua changamoto za wafuga nyuki wetu kule vijijini na kuongeza thamani ya asali yetu," alisema Mhe. Mongera.

***"Hivi ndivyo vyuo vyetu vinatakiwa kufanya. Siyo tu kutoa vyeti, bali kutoa wataalamu wenye ujuzi wa vitendo na uwezo wa kubuni vifaa vinavyoenda kutatua changamoto za wafuga nyuki wetu kule vijijini na kuongeza thamani ya asali yetu,"***

# SUA yazindua kitabu

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kupitia Mradi wa Timber Rush kimezindua kitabu Timber Rush: Private Forestry on Village Land in the Southern Highlands of Tanzania kinachotoa mwongozo kuhusu biashara ya miti, usimamizi wa misitu na uhifadhi wa mazingira.

Akizindua kitabu hicho, Naibu Makamu Mkuu Chuo, Prof. Maulid Mwatawala, alisema kitabu hicho kitasaidia kuimarisha sekta ya misitu kwa kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali za misitu, kuongeza kipato kwa jamii na kuchangia kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Mchapishaji wa kitabu hicho, Marc Ngotonie kutoka Mkuki na Nyota Publishers Ltd, alisema kitabu kinajumuisha matokeo ya tafiti za kisayansi, uzoefu wa utekelezaji na athari za kiuchumi za biashara ya miti, huku kikitarajiwa kuwa rejea muhimu kwa wasomi, watunga sera na wadau wa sekta ya misitu.

Mratibu wa Mradi wa Timber Rush, Prof. Dismas Mwaseba, alisema kitabu kimetokana na utafiti uliofanyika kati ya mwaka 2016 na 2021 kuhusu maendeleo ya upandaji miti nchini.

Aidha, mradi huo umechangia kujenga uwezo wa wanafunzi kwa kutoa mafunzo na kufanikisha wanafunzi wawili kupata shahada za uzamivu (PhD).
















# Serikali yaipongeza SUA kwa mchango wake katika kuendeleza kilimo Ikolojia nchini

Serikali imekipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa mchango wake katika kuendeleza kilimo ikolojia nchini, hususan kupitia ushirikiano wake na Wakfu wa McKnight uandaaji wa mtaala wa mafunzo kwa maafisa ugani.

Pongezi hizo zilitolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Prof. Peter Msoffe, wakati wa ufunguzi wa Jukwaa la Mwaka la Wadau wa Kilimo Ikolojia Tanzania lililofanyika Morogoro.

Alisema juhudi za SUA zina mchango mkubwa katika kuboresha huduma za ugani na kuongeza tija kwa wakulima.

Aidha, Prof. Msoffe amependekeza mtaala huo uanze kufanyiwa majaribio kwa kuwashirikisha wakufunzi wa Vituo vya Mafunzo ya Kilimo (MATI), ili kurahisisha uenezaji wa teknolojia za kilimo hai.

Pia alihimiza matumizi ya Kituo cha Mafunzo ya Wakulima cha Bihawana kwa ajili ya mafunzo ya vitendo.

Vilevile, alisisitiza umuhimu wa kuwashirikisha wakulima moja kwa moja kupitia mpango wa "Sauti ya Mkulima" utakaosaidia kukusanya maoni, changamoto na mapendekezo ya suluhisho kutoka kwa wadau wa msingi.

Serikali imeahidi kuendelea kushirikiana na taasisi za utafiti na vyuo vikuu katika kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kilimo Ikolojia Hai (2023–2030) ili kuimarisha usalama wa chakula na lishe nchini.



**Prof. Peter Msoffe**
Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo.





# Watafiti wa mradi wa NANOCOM watembelea wafugaji wa maziwa tanga kuimarisha sekta ya mifugo

Watafiti wa Mradi wa NANOCOM wamefanya ziara katika Mkoa wa Tanga kwa lengo la kutembelea wafugaji wa ng'ombe wa maziwa, kujionea shughuli za ufugaji zinazofanyika, kubadilishana uzoefu, pamoja na kujadili changamoto na fursa zilizopo katika sekta ya mifugo.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Prof. Gaymary Bakari, ambaye ni Kiongozi wa Mradi wa NANOCOM nchini Tanzania, alisema kuwa ziara hiyo ni sehemu muhimu ya shughuli za utafiti zinazolenga kupata uelewa wa kina kuhusu hali halisi ya ufugaji unaofanywa na wafugaji wa ng'ombe wa maziwa nchini. Alieleza kuwa matokeo ya utafiti huo yatachangia katika kuboresha uzalishaji wa mifugo na kuimarisha maendeleo ya sekta hiyo.

Prof. Bakari aliongeza kuwa mradi wa NANOCOM unalenga kuwajengea uwezo wafugaji kwa kutumia maarifa ya kisayansi na teknolojia za kisasa ili kuongeza uzalishaji wa maziwa, kuboresha afya ya mifugo na kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya dawa za mifugo.

Katika ziara hiyo, Prof. Xin Zhao kutoka Chuo Kikuu cha McGill, Kanada, alizungumza na wafugaji kuhusu masuala mbalimbali ya afya ya mifugo, hususan ugonjwa wa kiwele (mastitis), pamoja na madhara yatokanayo na matumizi yasiyo sahihi ya antibiotiki ambayo huchangia kuongezeka kwa usugu wa vimelea dhidi ya dawa.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa kuzingatia usafi wakati wa ukamuaji wa maziwa, matumizi sahihi ya dawa za mifugo na ufuatiliaji wa afya ya mifugo ili kuhakikisha uzalishaji wa maziwa salama na yenye ubora kwa matumizi ya binadamu.

Watafiti hao walitembelea wafugaji mbalimbali, akiwemo Dr. Sabath Benedict Mberesero wa Pongwe, Frank Mkanyu wa Mtaa wa Mafuriko, Kata ya Mzizima, pamoja na Mariam Shekuwe wa Pingoni Maweni. Katika ziara hizo, walipata fursa ya kujionea shughuli za ufugaji zinazofanyika na kujadiliana na wafugaji kuhusu changamoto zinazowakabili katika uzalishaji wa maziwa.

Kwa upande wao, wafugaji walieleza kufurahishwa na ujio wa watafiti hao, wakisema kuwa ziara hiyo imewapa maarifa mapya kuhusu mbinu bora za ufugaji, afya ya mifugo na njia salama na endelevu za kuongeza uzalishaji wa maziwa.

Naye Afisa Mkuu wa Mifugo wa Jiji la Tanga, Rashidi Chonga Nassoro, aliwashukuru watafiti wa Mradi wa NANO COM kwa kutembelea wafugaji wa mkoa huo. Alisema ziara hiyo imechangia kubadilishana uzoefu, kuimarisha ushirikiano kati ya watafiti na wafugaji na kuongeza uelewa kuhusu mbinu bora za ufugaji wa kisasa kwa maendeleo endelevu ya sekta ya mifugo nchini.









# Wataalamu wahimizwa matumizi ya kilimo ikolojia waonya athari za kemikali za kilimo

Wataalamu wa kilimo wameonya kuhusu ongezeko la matumizi holela ya kemikali za kilimo, wakisema hali hiyo inaweza kuhatarisha afya za binadamu, kuathiri ubora wa mazao na kusababisha uharibifu wa mazingira. Wametoa wito kwa wakulima kuzingatia kanuni za kitaalamu na kuhamia zaidi katika mbinu za kilimo ikolojia ili kuhakikisha uzalishaji endelevu na salama.

Akizungumza katika mkutano ulioandaliwa na Sekretarieti ya Kitovu cha Kilimo Ikolojia kupitia Mradi wa Mtandao wa Utafiti wa Ikolojia Kusini mwa Afrika (RAENS) mkoani Morogoro, Prof. Kalunde Sibuga wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) alisema matumizi yasiyo sahihi ya kemikali yanaweza kuathiri afya za wakulima na walaji, pamoja na kuacha mabaki hatarishi kwenye mazao.

Prof. Sibuga alieleza kuwa kilimo ikolojia ni mbinu muhimu inayochangia kuongeza uzalishaji kwa kutumia teknolojia na njia rafiki kwa mazingira, zikiwemo mbolea za asili, udhibiti wa wadudu kwa njia za kibaiolojia na usimamizi endelevu wa ardhi na maji. Alisisitiza umuhimu wa kuendelea kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi salama ya pembejeo za kilimo.

Kwa upande wake, Mratibu wa RAENS, Profesa Dismas Mwaseba, alisema licha ya kuwepo kwa sera zinazounga mkono kilimo endelevu, bado kuna changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa masoko ya uhakika, uelewa mdogo wa wakulima kuhusu kilimo ikolojia na upungufu wa huduma za mafunzo na ugani.

Naye mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Bw. Gosbert Chobya, alisema Serikali inaendelea kutambua mchango wa kilimo ikolojia katika kuongeza tija, kuhifadhi mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya Serikali, taasisi za utafiti na wadau wengine katika kuimarisha utekelezaji wa kilimo hicho nchini.










# SUA yaimarisha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa teknolojia ya mbao



Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Ki limo (SUA) wanaendelea kunufaika na miundombinu ya kisasa inayowawezesha kupata mafunzo kwa vitendo, yanayowaandaa kwa ufanisi kuingia katika soko la ajira kupitia programu mbalimbali za kitaaluma.

Akizungumza na SUA media, Mhadhiri Msaidizi kutoka Idara ya Uhandisi wa Misitu na Matumizi ya Mbao, Gabriel Mang'ula alisema mfumo huo wa mafunzo kwa vitendo unawasaidia wanafunzi kuunganisha maarifa ya nadharia wanayohifunza darasani na utekelezaji halisi wa kazi.

Alisema hatua hiyo inachangia kuongeza umahiri wao wa kitaaluma na kuwajengea uwezo na kushindana katika soko la ajira Katika mafunzo hayo, wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Shahada ya Teknolojia ya Mbao na Uongezaji wa Thamani walijifunza ukaushaji mbao kwa njia ya asili. Wanafunzi wa mwaka wa pili walifanya uchakataji wa magogo, huku wale wa mwaka wa tatu wakitengeneza samani mbalimbali kwa matumizi ya chuo.

Mazoezi hayo yalifanyika katika kiwanda cha Vuyisile Mini kilichopo Ndaki ya Solomon Mahlangu, ambapo wanafunzi hupata uzoefu wa moja kwa moja katika mazingira yanayofanana na yale ya viwandani kabla ya kuhitimu masomo yao.

# Mafunzo kwa vitendo katika sekta ya uvuvi yaendelea kuimarisha ujuzi wa wanafunzi wa SUA



Wanafunzi wa mwaka wa tano wa Shahada ya Kwanza ya Tiba ya Wanyama (BVM) kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wanaendelea kunufaika na mafunzo kwa vitendo yanayowaongezea ujuzi na uzoefu wa kitaaluma katika sekta ya uvuvi.

Mafunzo hayo yalifanyika katika Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Nyegezi, Mwanza pamoja na Maabara ya Taifa ya Uvuvi, chini uongozi wa Dkt. Lupindu kutoka Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya, Idara ya Tiba ya Wanyama na Afya ya Jamii.

Kupitia mafunzo hayo, wanafunzi walijifunza kwa kina namna sampuli mbalimbali zinavyopokelewa, kuchakatwa na kupimwa kwa kuzingatia viwango vya kitaalamu, hatua zinazochangia kuimarisha uwezo wao katika uchunguzi na udhibiti wa magonjwa ya viumbe wa majini.

Aidha, kupitia ushirikiano kati ya SUA na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Taanzania (TAFIRI), wanafunzi walipata fursa ya kujifunza hatua muhimu katika uzalishaji wa samaki ikiwemo ukusanyaji wa mayai, utotolewaji wa vifaranga, pamoja na mbinu za ukuzaji wa samaki, ikiwemo ukusanyaji wa mayai, utotoleshaji wa vifaranga, pamoja na mbinu za ukuzaji wa samaki kwa kutumia vizimba. Vilevile, walijifunza namna ubora wa maji unavyopimwa ili kuhakikisha mazingira yanayofaa kwa ukuaji bora na wenye tija wa samaki.



# SUA yaimarisha ujuzi wa kidijitali kwa wanafunzi na watumishi wa kilimo biashara



Wanafunzi na watumishi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) wamehimizwa kutumia kikamilifu fursa za mafunzo ya kielektroniki (e-learning) ili kuendeleza ujuzi wa kilimo biashara, kubuni miradi yenye tija na kuongeza uwezo wa kupata ufadhili pamoja na masoko ya ndani na kimataifa.

Akizungumza katika semina ya Agribusiness e-Academy Road Tour iliyoandaliwa na Shirika la GIZ kwa kushirikiana na SUA, Mkuu wa Idara ya Uchumi wa Kilimo na Biashara, Dkt. Fulgence Mishili, alisema chuo kinaendelea kuimarisha mifumo ya kidijitali inayowezesha ujifunzaji endelevu kwa wanafunzi na watumishi wakati wowote na mahali popote.




Dkt. Mishili alisema kuwa kupitia mifumo hiyo, washiriki wanaweza kuhudhuria kozi mbalimbali nje ya muda wa kawaida wa kazi au masomo na kupata vyeti vitakavyowaongezea sifa ya kushiriki katika miradi inayofadhiliwa na taasisi mbali mbali za kimataifa, ikiwemoUmoja wa Ulaya (EU) na GIZ.

Kwa upande wao, washiriki wa semina hiyo walisema mafunzo hayo yamewapanua uelewa kuhusu namna ya kubadili mawazo ya biashara kuwa miradi yenye tija, kuandaa maandiko ya miradi yanayokidhi vigezo vya wafadhili, pamoja na kutafuta na kuingia katika masoko yenye uhakika.



Mmoja wa washiriki, Fatuma Mmari, alisema mafunzo yamemuwezesha kuelewa hatua muhimu za kuanzisha mradi wa kilimo bishara na namna ya kukabiliana na changamotoza masoko.

Alibainisha kuwa changamoto ya ukosefu wa soko huwakwamisha wengi wanaoanza uzalishaji wa mazao au mifugo bila kuwa na maandalizi ya kutosha.

Naye mwanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Shahada ya Kilimo Biashara, Happyness Jacob Railo, alisema semina hiyo imemjengea ujasiri wa kuanzisha mradi wake binafsi na kuutangaza katika masoko ya kimataifa. Aliongeza kuwa sasa ana uelewa mzuri wa namna ya kuandaa wazo la biashara, kuliwasilisha kwa ufanisi na kuvutia ufadhili.



# Ndege nyuki kuwasaidia wanafunzi SUA kujifunza katika mazingira halisi ya kiteknolojia



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Rafael Chibunda amesema huo hicho kinaendelea kuboresha mbinu za ufundishaji kwa wanafunzi wake kwa kuanzisha matumizi ya teknolojia ya ndege nyuki (drones), hatua inayolenga kuwawezesha wanafunzi kujifunza katika mazingira halisi ya kiteknolojia.

Alisema kuwa Chuo kimeongeza matumizi ya teknolojia ya matrekta ili kurahisisha ufundishaji na kuwapa wanafunzi uzoefu wa moja kwa moja katika kilimo cha kisasa pamoja na matengenezo ya mitambo ya kilimo, hatua inayolenga kuzalisha wataalamu wenye ushindani zaidi.

Akizungumza katika mafunzo kwa vitendo yaliyofanyika mashambani, Rasi wa Ndaki ya Kilimo SUA, Dkt. Nyambilila Amuri, aliishukuru Menejimenti ya Chuo kwa kuona umuhimu wa kufundisha wanafunzi kwa vitendo.

Alisema matumizi ya drones yanafanyika kwa kushirikiana na kampuni ya Agrimazao, huku akibainisha kuwa hatua hiyo inalenga kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa mazao pamoja na kuwajengea wanafunzi ujuzi wa vitendo unaoendana na mahitaji ya soko la ajira.

Aliongeza kupitia matumizi ya drones, wanafunzi wanapata uelewa mpana wa teknolojia hiyo na hivyo kuwa tayari kuitumia hata wanapoajiriwa katika makampuni mbalimbali ya kilimo na biashara.



# Wanafunzi wa Mafiga Sekondari wapongeza SUA kwa kuimarisha mafunzo ya Amali

Wanafunzi wa Kidato cha Sita katika Shule ya Sekondari Mafiga wamekipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kuendelea kuimarisha mafunzo ya mkondo wa amali, wakisema yamewaongezea kupata ujuzi wa vitendo na unaowasaidia kuunganisha nadharia wanazojifunza darasani na mazingira halisi ya kazi .

Wakizungumza wakati wa mahafali ya tisa ya shule hiyo, baadhi ya wanafunzi akiwemo Saimon Justine Taibu na Iddy Silvan Malizia walisema ushirikiano na SUA umewapa maarifa na ujuzi katika maeneo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kilimo na uzalishaji wa mifugo. Wameeleza kuwa mafunzo hayo yayowaongezea uwezo wa kujitegemea na kuwaandaa vyema kwa ushindani katika soko la ajira.

Kwa upande wake, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Mafiga, Robert Marwa, aliishukuru SUA kwa mchango wake katika kuimarisha mafunzo kwa vitendo kupitia wataalamu wake na kuwezesha huduma za usafiri zilizorahisisha utekelezaji wa programu za mafunzo ya amali.

Akizungumza kwa niaba ya Mgeni rasmi, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Prof. Samweli Kabote, aliwahimiza wanafunzi kufanya bidii katika maandalizi ya mitihani yao ya mwisho ili kufikia malengo yao ya kitaaluma na maisha.



# Serikali inaendelea kuweka mazingira rafiki ya kuwawezesha vijana kiuchumi, Waziri Nanauka

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais anayeshughulikia Maendeleo ya Vijana, Mhe. Joel Nanauka amesema Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuwawezesha vijana kiuchumi kupitia mipango mbalimbali, ikiwemo mikopo ya asilimia 10 inayotengwa na halmashauri nchini, ili kuwasaidia vijana kujitegemea na kushiriki katika maendeleo ya Taifa.

Akizungumza katika uzinduzi wa Jukwaa la Vijana la Platform Campus Connect Mkoa wa Morogoro lililofanyika Kampasi ya Solomon Mahlangu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo(SUA), Mh. Nanauka aliema Serikali inaendelea kuboresha mifumo ya utoaji wa mikopo hiyo ili vijana wengi zaidi waweze kunufaika kwa urahisi.

Aidha, aliwahimiza vijana kutumia fursa hizo kwa ubunifu, uwajibikaji na nidhamu ya matumizi ya fedha.

Kwa niaba ya vyuo vya elimu ya juu ya Mkoa wa Morogoro, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) anayeshughulikia Utawala, Fedha na Mipango, Prof. Amandus Muhairwa, alisema taasisi za elimu ya juu zina jukumu la kuwajengea vijana maarifa, ubunifu na stadi za ujasiriamali ili wawe viongozi, wabunifu na wachochezi wamaendeleo ya Taifa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Japhari Kubecha, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, alisema Mkoa huo utaendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za kuwawezesha vijana kiuchumi na kijamii, akisisitiza kuwa vijana ndio muhimu ya maendeleo endelevu ya Taifa.




**Mhe. Joel Nanauka**
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais anayeshughulikia Maendeleo ya Vijana.











# SUA, AFIDA na IFA watoa mafunzo ya mbolea endelevu kuimarisha kilimo Afrika

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kwa kushirikiana na Africa Fertilizer Industry Development Association (AFIDA) na International Fertilizer Association (IFA), kiliendesha mafunzo maalum kuhusu matumizi endelevu ya mbolea na afya ya udongo, yakilenga kuwajengea uwezo wahitimu wa fani za kilimo ili kuongeza uzalishaji wenye tija na endelevu barani Afrika.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, Rasi wa Ndaki ya Kilimo ya SUA, Dkt. Nyambilila Amuri, alisema ushirikiano kati ya taasisi hizo una mchango mkubwa katika kuimarisha ubora wa elimu, utafiti na mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa fani za kilimo.

Dkt. Nyambilila alisema mafunzo hayo yanawawezesha washiriki kupata maarifa na ujuzi wa vitendo kuhusu matumizi sahihi ya mbolea na usimamizi wa afya ya udongo, hatua inayowaandaa vyema kukabiliana na changamoto za sekta ya kilimo na mahitaji ya soko la ajira.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa AFIDA, Dkt. Innocent Okuku, alisema mafunzo hayo ni sehemu ya jitihada za kuisaidia Afrika kujitosheleza kwa chakula kupitia ongezeko la uzalishaji wa ndani na kupunguza utegemezi wa uagizaji kutoka nje.

Alisisitiza umuhimu wa matumizi sahihi na endelevu ya mbolea ili kuongeza tija ya uzalishaji wa mazo, kuboresha afya ya udongo na kuimarisha usalama wa chakula kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Wanafunzi walioshiriki mafunzo hayo walieleza kuwa yamewaongezea uelewa wa kina kuhusu afya ya udongo, matumizi bora ya mbolea na mbinu za uzalishaji endelevu. Wamesema maarifa waliyoyapata yatawawezesha kutoa ushauri kwa wakulima na kuchangia kuongeza uzalishaji wa mazao katika jamii.

Mafunzo hayo yanaakisi dhamira ya SUA ya kuendelea kushirikiana na taasisi mbali mbali zikiwemo za kimataifa katika kuandaa wataalamu wenye ujuzi, weledi na uwezo wa kutumia sayansi na ubunifu kuleta maendeleo endelevu katika sekta ya kilimo barani Afrika.





# Wanafunzi wa Udaktari wa Mifugo SUA Wapata Mafunzo kwa Vitendo Katika Uhifadhi wa Wanyamapori

Baadhi ya wanafunzi wa mwaka wa tano SUA Shahada ya Udaktari wa Mifugo (Bachelor of Veterinary Medicine) walifanya mafunzo kwa vitendo katika maeneo ya uhifadhi wa wanyamapori.

Mafunzo hayo yaliwapa fursa ya kujifunza moja kwa moja katika mazingira halisi ya kazi na kukutana na changamoto mbalimbali za kitaalamu.

Katika kipindi cha mafunzo hayo, wanafunzi walishiriki katika shughuli mbalimbali za kitaalamu ikiwemo kuwalaza (immobilization) wanyamapori kama tembo, nyumbu, simba na pundamilia pamoja na kuwafanyia uchunguzi na vipimo mbalimbali vya afya.

Uzoefu huo uliwawezesha kuimarisha uelewa wao wa vitendo katika tiba na usimamizi wa afya za wanyamapori.

Lengo kuu la mafunzo hayo ni kuwajengea wanafunzi ujuzi wa vitendo katika usimamizi wa afya za wanyamapori, utambuzi wa magonjwa, pamoja na kuchangia juhudi za uhifadhi wa bioanuwai.





# Tathmini mapato ya kaboni yaangaliwa kama njia endelevu ya kufadhili uhifadhi wa misitu ya jamii Tanzania




Warsha ya kuwasilisha matokeo ya awali ya Mradi wa Tathmini ya Mapato ya Kaboni kama Njia Endelevu ya Uwezeshaji Kifedha katika Uhifadhi wa Misitu ya Jamii Tanzania imefanyika mkoani Dodoma, ikiwa na lengo la kujadili fursa na changamoto za kutumia biashara ya kaboni kama nyenzo ya kuimarisha uhifadhi wa misitu ya jamii.

Mgeni rasmi katika warsha hiyo alikuwa Rasi wa Ndaki ya Misitu, Wanyamapori na Utalii wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Agnes Sirima

Warsha hiyo iliwakutanisha wadau mbalimbali w wawakilishi wa taasisi za kiserikali, asasi za kiraia, taasisi za kitaaluma na utafiti, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), pamoja na wawakilishi wa wananchi kutoka wilaya za Mvomero, Korogwe, Mwanga, Mbulu na Tanganyika.

Akizungumza katika warsha hiyo, Prof. Sirima alisema mradi  huo unalenga kutathnini uwezekano wa kutumia mapato yatokanayo na biashara ya kaboni kama njia endelevu ya kifedha ya kuimarisha uhifadhi wa misitu ya vijiji, kulinda bioanuai, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na kuboresha maisha ya jamii kupitia usimamizi shirikishi wa misitu.

"Mradi huu unafanya utafiti kuangalia uwezekano wa kutumia mapato ya kaboni kama mpango endelevu wa kifedha ili kuimarisha uhifadhi wa bioanuai, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na kuboresha maisha ya jamii kupitia Usimamizi Shirikishi wa Misitu." alisema Prof. Sirima.

Kwa upande wake, Kiongozi wa Mradi huo, Dkt. Kajenje Magessa,  alisama warsha hiyo imelenga kuwasilisha matokeo ya awali ya utafiti kwa wadau mbalimbali, wakiwemo taassisi binafsi, taasisi za kiserikali na wawakilishi wa wananchi.

Alisema matokeo hayo yaliwasilishwa kupitia mada mbalimbali zikiwemo  Forest Governance Status iliyowasilishwa na Dkt. Kajenje Magessa, Forest Carbon Potentialiliyowasilishwa na Dkt. Paulo Lyimo, Cost and Benefits (Opportunity Costs) for Carbon Trading" iliyowasilishwa na Dkt. Neal Hockley, pamoja na Capacity Needs Gaps in Carbon Trading iliyowasilishwa na Prof. Gimbage Mbeyale.

Dkt Kajenje aliongza kuwa hatua inayofuata ni kuwajengea uwezo wadau katika ngazi mbalimbali ili waweze kufanya maamuzi sahihi kuhusu jinsi ya kunufaika na masoko ya kaboni katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kulinda bioanuai na koboresha maisha ya jamii zinazoishi katika maeneo ya misitu.

Naye Prof. Gimbage Mbeyale, ambaye ni miongoni mwa watafiti katika mradi huo, alisema matokeo ya awali yanaonesha kuwa katika maeneo ya Mbulu na Tanganyika, licha ya baadhi ya vijiji kuanza kunufaika na biashara ya kaboni, bado kuna uhitaji wa kuongeza uelewa wa viongozi na wananchi kuhusu utawala wa misitu, biashara ya kaboni na taratibu zake.

Alisisitiza umuhimu wa kuendelea kutoa elimu kwa jamii ili kuhakikisha jamii  zinafuata sera na sheria zilizopo, huku akieleza kuwa biashara ya kaboni inazingatia misingi ya kisayansi na inalenga kutoa manuafaa kwa wote wanaoshiriki katika uhifadhi bila upendeleo.

Kwa upande wake, Bw. Isaac Emmanuel kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), alisema mradi huo ni muhimu kwa serikali kwa kuwa utaongeza uelewa wa wananchi kuhusu usimamizi wa misitu na kutoa fursa za kiuchumi kwa jamii zinazoshiriki katika shughuli za uhifadhi.

Wananchi kutoka baadhi ya vijiji ambavyo bado havijaanza kunufaika na biashara ya kaboni walielezea matumaini yao ya kujiunga na mpango huo, wakivutiwa na mafanikio ya kiuchumi yanayoonekana katika maeneo ambayo tayari yameanza kupata mapato kupitia biashara hiyo.



# SUA na Messina wapo hatua ya mwisho kuanzisha Programu pacha

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Chuo Kikuu cha Messina (UniMe) cha Italia vipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mitaala na makubaliano yatakayowezesha kuanzishwa kwa programu za Shahada Pacha (Joint Double Degrees) na Stashahada za Uzamili kwa ushirikiano wa kimataifa.

Mpango huo ni sehemu ya mradi wa Erasmus+ Mobility Programme 2023–2026 unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya, unaolenga kuimarisha mabadilishano ya wanafunzi na watumishi katika maeneo ya tiba ya wanyama, uzalishaji wa mifugo na afya ya jamii (One Health).

Akizungumza wakati wa ziara ya ujumbe kutoka Italia, Rasi wa Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya, Prof. Esron Karimuribo, alisema vyuo hivyo tayari vina ushirikiano imara unaojumuisha mabadilishano ya wataalamu pamoja na wanafunzi wa uzamili na uzamivu, huku rasimu ya makubaliano ya programu hiyo ikiwa katika hatua za mwisho za kuboreshwa na kupitishwa.

Naye Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Utawala, Fedha na Mipango), Prof. Amandus Muhairwa, akimwakilisha Makamu Mkuu wa Chuo, alisema ushirikiano huo utaongeza kasi ya maendeleo ya SUA kwa kunufaika na uzoefu mkubwa wa taasisi kongwe kama Chuo Kikuu cha Messina katika kukabiliana na changamoto za maendeleo na uendeshaji wa mifumo.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Messina, Prof. Antonino Germanà, alisema Chuo hicho kimekuwa na ushirikiano wa muda mrefu na vyuo mbalimbali barani Afrika, hususan Afrika Kaskazini, na kwamba ushirikiano unaoanzishwa na SUA utakuwa wa kwanza nchini Tanzania na unafungua ukurasa mpya wa mahusiano ya kitaaluma kati ya taasisi hizo mbili.









# Waziri Kabudi asisitiza umuhimu wa kuimarisha huduma za afya ya uzazi, elimu na utafiti katika taasisi za elimu ya juu

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Watu Wenye Ulemavu), Prof. Palamagamba Kabudi amesisitiza umuhimu wa kuimarisha huduma za afya ya uzazi, elimu na utafiti katika taasisi za elimu ya juu ili kuwaandaa vijana kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya taifa.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na vyuo vikuu kuhakikisha huduma rafiki za afya zinapatikana kwa vijana ili kupunguza maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI.

Prof. Kabudi aliyasema hayo alipotembelea Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), ambapo alizindua mashine za kisasa za kugawa bidhaa za kinga dhidi ya VVU na UKIMWI pamoja na huduma za upimaji wa VVU kwa siri.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda alitoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Afya kwa kuendelea kuunga mkono mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI.

Alisema msaada huo umeimarisha kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa programu za afya, elimu ya kinga na huduma rafiki kwa wanajumuiya wa Chuo.









# Wajumbe wa Baraza SUA wajengewa uwezo kuimarisha uongozi na utawala bora

Wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wanaendelea kushiriki mafunzo maalumu ya kuwajengea uwezo katika utekelezaji wa majukumu yao ya kiutawala na kimkakati, kwa lengo la kuimarisha uongozi, utawala bora na uwajibikaji ndani ya Chuo. Mafunzo hayo yanatolewa na Taasisi ya Uongozi na yanafanyika katika Hoteli ya Cate, mkoani Morogoro.

Akifungua mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Mhe. Andrew Massawe, aliwataka wajumbe kuyatumia mafunzo hayo kama fursa ya kuongeza maarifa na kubadilishana uzoefu ili kuimarisha uwezo wao wa kusimamia Chuo kwa kuzingatia misingi ya utawala bora, uwazi na uwajibikaji.

Akiwasilisha mada kuhusu Uongozi Shirikishi na Utoaji wa Mwongozo katika Utawala, mwezeshaji wa mafunzo hayo, Dkt. Kassim Hussein, alieleza kuwa uongozi shirikishi ni nguzo muhimu katika mafanikio ya taasisi. Alibainisha kuwa viongozi wa Kurugenzi, Vitengo na Idara mbalimbali wanayo maarifa na uzoefu unaokamilishana, hivyo ushirikishwaji wao katika kufanya maamuzi huimarisha mshikamano, huongeza uwajibikaji na huleta ufanisi katika utekelezaji wa mipango na majukumu ya Chuo.

Katika mafunzo hayo, wajumbe pia walijengewa uelewa kuhusu usimamizi wa rasilimali za Chuo, wakikumbushwa wajibu wao wa kuhakikisha rasilimali hizo zinasimamiwa kwa uadilifu, uwazi na ufanisi ili ziweze kutumika kikamilifu katika kufanikisha malengo ya Chuo na kuhudumia maslahi ya wadau wake.

Mafunzo hayo yanatarajiwa kuimarisha uelewa wa pamoja kuhusu wajibu na majukumu ya Baraza la Chuo, kuboresha ushirikiano katika kufanya maamuzi ya kimkakati na kuendelea kuimarisha misingi ya uongozi na utawala bora kwa maendeleo endelevu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.










# Watumishi wa SUA wakumbushwa kuweka akiba na kuwekeza kwa ajili ya maisha ya baadaye









Watumishi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wamehimizwa kutumia vipato vyao kwa busara, kuweka akiba na kuwekeza katika miradi yenye tija ili kujenga uhuru wa kifedha na kujiandaa kwa maisha ya baada ya kustaafu.

Akizungumza kwa niaba ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Fedha, Mipango na Utawala, Prof. Damas Philipo, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya usimamizi wa fedha kwa watumishi yaliyofanyika katika Kampasi ya Edward Moringe, mkoani Morogoro, alisema usimamizi bora wa fedha ni msingi muhimu wa mafanikio ya mfanyakazi.

Alieleza kuwa usimamizi huo huchangia ustawi wa mtu binafsi, familia na jamii kwa ujumla.

Prof. Philipo aliwahimiza washiriki kutumia maarifa watakayopata katika mafunzo hayo kubadili mtazamo kuhusu matumizi ya fedha, kujenga utamaduni wa kuweka akiba na kuwekeza, ili waweze kufikia malengo yao ya muda mfupi na ya muda mrefu.

Kwa upande wake, Mkaguzi Mwandamizi kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Bw. Edward Clement, alisema mfuko huo una jukumu la kuhakikisha watumishi wanapata hifadhi ya jamii na kuwa na maisha yenye uhakika baada ya kustaafu.

Mafunzo hayo pia yalihudhuriwa na wadau mbalimbali, wakiwemo wawakilishi wa Benki ya NMB na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), ambao waliwasilisha mada mbalimbali kuhusu usimamizi wa fedha, uwekezaji na huduma za hifadhi ya jamii.



# Ushirikiano wa SUA na APOPO waendelea kukua, maabara ya muda ya uchunguzi wa kifua Kikuu yapendekezwa kujengwa Olmontonyi

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimepokea ombi kutoka Shirika lisilo la Kiserikali la Apopo la kujenga maabara ya muda ya uchunguzi wa kifua kikuu katika eneo la Chuo, Msitu wa Mafunzo wa Olmotonyi, jijini Arusha, ikiwa ni hatua ya kuendeleza ushirikiano wa muda mrefu kati ya taasisi hizo mbili.

Akizungumza katika kikao na Menejimenti ya Chuo, Mkurugenzi Mtendaji wa Apopo, Bw. Christophe Cox, alisema maabara hiyo ya muda inapendekezwa kujengwa kwa lengo la kuimarisha shughuli za uchunguzi na utafiti wa ugonjwa wa kifua kikuu.

Kwa niaba ya Menejimenti ya Chuo, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael T. Chibunda, alisema SUA imepokea ombi hilo na kwa sasa linaendelea kufanyiwa kazi kwa kuzingatia taratibu za Chuo.

Apopo na SUA zimekuwa na ushirikiano wa karibu kwa muda mrefu katika nyanja za utafiti na mafunzo. Kwa sasa, shirika hilo linatumia eneo la SUA katika Kampasi ya Edward Moringe, ambako lina ofisi pamoja na miundombinu ya kuwafunza panya maalum wanaotumika katika shughuli za uchunguzi wa kifua kikuu na magonjwa mengine.

Iwapo ombi hilo litapitishwa, maabara hiyo ya muda itakuwa hatua nyingine ya kuimarisha ushirikiano kati ya SUA na Apopo katika kukuza utafiti, ubunifu na mchango wa pamoja katika sekta ya afya.



# Wanafunzi SUA wahimizwa kupima afya mara kwa mara kujua hali zao











Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, SUA wametakiwa kujenga tabia ya kupima afya mara kwa mara ili kujua hali zao mapema, hasa kwa magonjwa yasiyoambukiza ambayo mara nyingi hayatoi dalili za haraka.

Akizungumza kwenye bonanza la kuhamasisha upimaji wa afya na uchangiaji damu lililofanyika Kampasi ya Edward Moringe, Dkt. Erhard Kapilima alisema utambuzi wa mapema husaidia kuanza matibabu kwa wakati na kuokoa maisha.

Mbali na upimaji wa afya, wanafunzi pia walijitokeza kuchangia damu kwa ajili ya kusaidia wagonjwa wenye uhitaji mkubwa wa damu, wakiwemo wanawake wajawazito wanaojifungua.

Aidha, Dkt. Kapilima aliwahimiza wanafunzi kujiepusha na tabia hatarishi zinazoweza kusababisha maambukizi ya Virusi vya Ukimwi na magonjwa mengine ya kuambukiza.









# MATANGAZO

## KARIBU UTANGAZE NA SUA FM, 101.1

*Kwa Gharama Nafuu*




*@sokoineuniversityofagriculture*

*@SokoineU*

*Kwa Mawasiliano piga simu*

**0655424251**
**0655370047**

# UTALII

## KARIBU UTEMBELEE KAMPASI ZA SUA KWA UTALII NA KUJIFUNZA















**Jarida limeandaliwa na:**
Kitengo cha Mawasiliano na Masoko
S.L.P 3000, Chuo Kikuu, Morogoro, Tanzania
Simu: 255-023-2640006/7/8/9,
Baruapepe: communicationandmarketing@sua.ac.tz